



Kwanini Matandazo?

Bila matandazo...



Matandazo...



Huhifadhi unyevunyevu

Wakati wa kiangazi unyevunyevu hupotea, udongo hukauka, kuwa mgumu na kukatika.

Matandazo huzuia kupotea kwa unyevunyevu na kuhifadhi unyevunyevu kwenye udongo.

Zuia magugu

Magugu huchukua mwanga na rutuba kutoka kwenye udongo.

Matandazo huzuia magugu kuota, hivyo kuwa na mwanga na rutuba kwaajili ya mimea.

Huzuia mmomonyoko

Matone ya mvua yanapodondoka huosha udongo wa juu na kuacha mifereji. Matandazo hukinga udongo kwa kufanya maji yaingie taratibu.

Namna ya kuweka matandazo

Nitumie nini?

Tumia masalia ya mimea kama vile migomba, mabua ya mahindi, maharage, majani na magugu kuweka matandazo. Usitumie mimea iliyoathirika kwani inaweza kusambaza maradhi ya ugonjwa.

Vipi wadudu waharibifu?

Acha nafasi kuzunguka shina la mmea ili kuzuia wadudu waharibifu.

Lini niweke matandazo?

Weka matandazo kila mara wakati wa kiangazi ili kufanya udongo uwe na unyevunyevu. Wakati wa masika matandazo huzuia mmomonyoko na magugu.

Matandazo huongeza mboji/matamahuruku kwenye udongo hivyo kuuboresha na kuongeza mazao.

Matandazo hufanya mimea iwe na afya, na huongeza mboji/matamahuruku ambayo huboresha udongo na huongeza mazao.